na ugonjwa huo.
Hiyo ni sehemu ya

Alitoa pongezi hizo
baada ya kupokea taarifa ya

HABARI LEO UK 7.

# Serikali yahimiza viwanda vya uvuvi

**Na Mwandishi Maalumu, Sengerema**

SERIKALI imesema inataka kuona uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya wafugaji na wavuvi kupitia mikopo inayotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili kuyaongezea thamani mazao yanayotokana na sekta za mifugo na uvuvi.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alizungumza hayo mwishoni mwa wiki katika Kijiji cha Kanyala kilichopo Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Alikuwa akikabidhi mkopo wa Sh milioni 100.7 uliotolewa na TADB kwa Chama cha Ushirika cha Zilagula ambacho pia kimepata mkopo wa Sh milioni tano kutoka katika mfuko wa mapato ya ndani ya halmashauri hiyo.

Ulega alisema licha ya vyama vingine vya Kasalazi na Soswa ambavyo kila kimoja kimepata pia mkopo wa halmashauri wa Sh milioni tano ili wafugaji na wavuvi wanufaike na mikopo kupitia ushirika wao, wizara itakuwa msimamizi kwa vyama vitakavyokidhi sifa za kupata mikopo kutoka TADB.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaenda kuwa msimamizi namba moja wa vyama vya ushirika tena kwa barua hivyo niwatakeni uongozi wa mkoa, halmashauri na ushirika wekeni taarifa zenu vizuri.

"Tunataka viwanda vidogo vidogo vya wafugaji na wavuvi vikiwemo vya kukausha dagaa, minofu ya samaki na kutengeneza kayabo nzuri ili mpeleke bidhaa hizo kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema Ulega.

Alivitaka vyama hivyo vitatu vilivyopata mikopo waitunze kwa kuifanyia kazi na hatimaye kuirejesha, kwa kuwa fedha zilizotolewa na benki hiyo zinamilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100 ili wengine pia wanuifaike nayo.

Alitoa rai kwa wavuvi kuendelea kujiunga katika vyama vya ushirika wakati akikabidhi hati ya kuandikishwa kwa vyama vya Sangara-Nyakaliro na Gembare vilivyopo Halmashauri ya Buchosa.

Aliwataka pia watendaji wa serikali kutoa elimu kwa vyama vya ushirika namna ya kuitumia vyema mikopo wanayopata ili wairejeshe kwa wakati pamoja na kuwaongoza ili wapate mikopo mikubwa zaidi.

Pia aliwataka viongozi wa vyama vya ushirika kujiepusha na ubadhirifu wa fedha za mikopo, huku akitoa rai kwa wavuvi kuwa na uchumi endelevu na hatimaye kuwa walinzi wa rasilimali za uvuvi kupitia vyama vyao.

Alisema azma ya serikali ni kuona Tanzania inaongoza kwa kusafirisha minofu ya samaki kwenda nje ya nchi na mchango wa samaki katika Pato la Taifa unaongezeka kutoka asilimia 1.7 hadi 2 na kufikia asilimia tano na zaidi.

Scanned with CamScanner

# Wafugaji nchini wapewa siku 30 kufanya uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi imetoa siku 30 kufanyika uchaguzi wa viongozi kwa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), baada ya viongozi waliopo madarakani kumaliza muda wa ukomo wao tangu mwaka 2018.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ramadhani Kailima kwa niaba ya Katibu Mkuu, chama hicho kimeingia kwenye mchakato huo baada ya wizara hiyo kutoa maelekezo uchaguzi wa viongozi wa chama hicho ufanyike ndani ya siku 30 kuanzia leo.

Kailima alisema ili kuwezesha kufanyika kwa uchaguzi huo, kutakuwepo kwa kamati ya kuratibu uchaguzi yenye wajumbe kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi itakayofanya kazi na Tume ya Uchaguzi itakayochaguliwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu.

Aidha, alisema Juni 4, kutafanyika mkutano mkuu wa chama hicho jijini Dodoma kwa ajili ya kujipatia, kujadili na kupitisha majina ya wajumbe wa tume ya uchaguzi watakaosimamia mchakato wa uchaguzi.

Alisema Juni 27 hadi 28, mwaka huu, tume hiyo ya uchaguzi itafanya mchujo wa wagombea wa nafasi mbalimbali, kupokea pingamizi na kufanya maamuzi ya pingamizi.

Alisema Juni 29, mwaka huu, kutafanyika mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa chama hicho utakaofanyikia jijini Dodoma na Juni 30, mwaka huu yatafanyika makabidhiano ya uongozi.

Naibu Katibu Mkuu alisema kwa mujibu wa Katiba ya chama hicho, uchaguzi wa viongozi wa CCWT unapaswa kufanyika kila baada ya miaka mitatu, na chama hicho kilipanga kufanya uchaguzi wake Desemva 16, 2018.

"Lakini uchaguzi huo hakufanyika kama ulivyopangwa baada ya zuio la Msajili wa Jumuiya za Kijamii kutokana na malalamiko yaliyowasilishwa na baadhi ya wanachama kuhusu kukiukwa kwa taratibu za uchaguzi kwa mujibu wa Katiba ya chama," alisema Kailima.

Alisema kutokana na muda mrefu wa viongozi hao kukaa madarakani, wanachama wa chama hicho, waliwasilisha malalamiko yao kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakitaka kufanyika uchaguzi jambo ambalo sasa limefanyiwa kazi.

ewura

Dk Zainab ahimiza

Scanned with CamScanner

# TADB yakopesha wavuvi Sh mil 100.7

Na MWANDISHI WETU
- SENGEREMA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), imetoa mkopo wa Sh milioni 100,7 kwa Chama cha Ushirika cha Zilagula kilichopo Buchosa wilayani Sengerema ili kununua zana bora za uvuvi zitakazowasaidia kuongezamitaji,kupunguza upotevu wa samaki na kuongeza uthamani wake ili kuwanufaisha wavuvi na kukuza uchumi.

Akizumgumza wakati akikabidhi hundi hiyo mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi,Abdallah Ulega alisema Serikali inataka kuona uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya wafugaji na wavuvi kupitia mikopo inayotolewa na benki ili kuyaongezea thamani mazao yanayotokana na sekta za mifugo na uvuvi sambamba na kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi.

Aliwataka viongozi wa vyama vya ushirika kujiepusha na ubadhilifu wa fedha za mikopo hiyo kutoka TADB, huku akitoa rai kwa wavuvi kuwa na uchumi endelevu na hatimaye kuwa walinzi wa rasilimali za uvuvi kupitia vyama vyao vya ushirika kwa kuwa azma ya serikali ni kuona Tanzania inaongoza kwa kusafirisha minofu ya samaki kwenda nje ya nchi na mchango wa pato la taifa unaongezeka kutoka Asilimia 1,7 hadi 2 ya sasa na kufikia asilimia tano na kuendelea.

Pia aliwataka watendaji wa Serikali kutoa elimu kwa vyama vya ushirika namna ya kuitumia vema mikopo wanayopata ili waweze kuirejesha kwa wakati.

Alisema wakifanya vizuri wanaweza kupata mikopo mikubwa zaidi kwa kuwa utoaji mikopo kwa vyama vya ushirika vya wafugaji na wavuvi ni maono ya Rais Dk. John Magufuli.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi, itaendelea kuwa msimamizi namba moja wa vyama vya ushirika tena kwa barua hii, nautaka uongozi wa mkoa, halmashauri na ushirika wekeni taarifa zenu vizuri,tunataka viwanda vidogo vidogo vya wafugaji na wavuvi vikiwemo vya kukausha dagaa, minofu ya samaki na kutengeneza kayabo nzuri ili mpeleke bidhaa hizo kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema

Mkurugenzi Mkuu wa TADB, Japhet Justine aliishukuru wizara kwa kuweka mikakati mizuri na benki hiyo iliyowezesha kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha wafugaji na wavuvi wanakuwa na sifa za kupatiwa mikopo ili kujiendeleza katika sekta hizo.

"Tuliomba kwanza vyama hivi vikae katika ushirika kwa sababu tuliamini ule umoja wao utatupatia njia kuhakikisha mikopo inalipwa kwa kuwaweka katika mfumo ulio rahisi, wizara pia iliweka mazingira wezeshi ili benki iweze kuwa na taarifa sahihi ya mitumbwi ya wahusika wanaopatiwa mikopo,"alisema.

Alisema ni wakati wa kuondokana na dhana iliyokuwapo ya wavuvi kutokopesheka. Serikali ya awamu hii imejikita imetengeneza mifumo mizuri ya fedha hivyo amevisisitiza vyama vya ushirika vilivyonufaika na mkopo kuhakikisha vinalipa mikopo hiyo kwa wakati ili Watanzania wengine wenye uhitaji waweze kupata na kukuza biashara zao.


Mratibu wa Dawati La Sekta Binafsi lililo chini ya wizara hiyo, Steven Michael alisema kazi yao kubwa ni kuhakikisha matokeo chanya yanaonekana likiwemo tukio Zilagula kupatiwa mkopo mnono.

Katibu Tawala Wilaya ya Sengerema, Alan Augustine alisema wilaya hiyo inakadiriwa kuwa na wavuvi 20,080, huku mitubwi ikiwa 5,020 shughuli za sekta hiyo zimekuwa zikiendelea kufanyika halmashauri zote mbili, huku elimu ikitolewa kwa wavuvi juu ya umuhimu wa kutunza rasilimali kuwa endelevu kwa kizazi cha leo na kijacho.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Crispin Luanda alisema kwa kutambua mchango wa sekta hiyo, wametoa Sh milioni 15 kutoka mapato yao ya ndani kwa vyama vitatu vya ushirika ambavyo ni Zilagula,Kasalazi na Soswa ambapo kila chama kilijipatia Sh milioni 5

Mwenyekiti wa Zilagula, Joram Yuda aliishukuru Serikali kwa kuwa wavuvi wameanza kuaminika na taasisi za kifedha kwa kupatiwa mikopo ili kujiendeleza.

– PICHA: MPIGAPICHA WETU




**HUNDI: Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Japhet Justine (wa pili kushoto), wakikabidhi mfano wa hundi ya mkopo wa sh million 100.7 kwa viongozi wa Chama cha Ushirika cha Zilagula wilayani Sengerema mkoani Mwanza mwishoni mwa wiki.**

# Changamkieni fursa usambazaji gesi

Na HADIJA OMARY

WAZIRI wa Nishati Dkt, Merdad Kalemani amewataka Watanzania kuchangamkia fursa ya mradi wa usambazaji wa gesi asilia majumbani kwa kuunganisha katika nyumba zao,taasisi na maeneo ya biashara kwa kuwa mpango huo unafaida lukuki.

Waziri Kalemani aliyasema hayo juzi, wakati wa uzinduzi wa mradi wa gesi asilia majumbani , viwandani na kwenye magari mkoani Lindi.

Alisema umefika wakati sasa wananchi wa mkoa huo na maeneo mengine yaliyopitiwa na mradi kuchangamkia fursa hiyo kwa sababu inapatikana kwa gharama nafuu.

Alisema kama mtu anatumia gesi asilia hupata punguzo la zaidi ya asilimia 45 ya gharama ambazo ungetumia kwenye vyanzo vingine kama vile gesi ya mtungi (NLG),mkaa,kuni au mafuta ya taa.

"Manufaa ya kutumia gesi asilia ni mengi, inapunguza gharama ukilinganisha na nishati zingine kama kuni na mkaa, kupunguza usumbufu wakati wa upatikanaji wake, inaimalisha familia na inainua uchumi lakini mtaalamu pia amesema haina hasara na hailipuki,"aliesema.

Aliwatoa hofu wananchi watakaopenda kutumia huduma hiyo juu ya gharama ya uunganishwaji ya kwamba kwa sasa gharama za uunganishaji, ni bure na mtumiaji atapaswa kulipia gharama ya matumizi pekee kulingana na matumizi yake.

Mkurugenzi mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dk.James Mataragio aliwatoa hofu watumiaji wa gesi, kuwa ni salama zaidi kuliko gesi ya mitungi (NLG) mafuta ya taa na kuni.

Alisema usalama wa gesi asilia unatokana na gesi kuwa nyepesi kuliko hata hewa inayovutwa na binadamu.

Scanned with CamScanner

UWEZESHAJI

## Wizara ya Mifugo yawezesha machinjio

Na MWANDISHI WETU
- ARUSHA

**WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imetoa vitendeakazi vya mazao ya mifugo kwa wachunaji wa ngozi kwenye machinjio yote ya Mkoa wa Arusha kwa ajili ya kuongeza thamani na kuboresha uchunaji wa ngozi.**

**Akikabidhi vifaa hivyo kwa Kaimu Katibu Tawala wa mkoa huo kwa niaba ya wachunaji hao, Mkurugenzi wa Masoko na Uzalishaji wa wizara, Felix Nandonde alisema kwa kipindi kirefu ngozi zimekuwa zikiharibiwa ubora wake kwa matumizi ya vifaa visivyo na ubora.**

**Alisema wizara ilitoa mafunzo ya siku moja kwa wachunaji wa ngozi mkoa huo ili kuboresha thamani ya ngozi, ikiwemo kutoa leseni kwa kila mchunaji na vifaa hivyo kwa lengo la kuongeza ubora kwenye kazi zao.**

**Alivitaja vitendea kazi kuwa, ni visu vya kisasa ambavyo vimetengezwa kwa teknolojia ya kisasa na vitatolewa bora kwa wachunaji wa Mkoa wa Arusha na nchini kote.**

**"Kwa kipindi kirefu sekta ya uchunaji,imekuwa ikionekana haina mwenyewe lakini sasa kupitia Serikali, imeanza kutambulika kwa lengo la kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo," alisema.**

**Akizungumza baada ya kupokea vifaa hivyo, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, David Lyamongi alipongeza wizara hiyo kutoa mafunzo kwa wachunaji na vitendeakazi hivyo.**

**Alisema vitendea kazi hivyo, vitawezesha mkoa kuzalisha ngozi zenye ubora wa hali ya juu na hivyo ngozi zitakuwa na thamani kubwa na masoko ya hali ya juu.**

**Alisema mkoa huo ambao ni wa wafugaji, vifaa vimekuja wakati muafaka kusaidia kuondokana na matumizi ya vifaa butu ambavyo vilikuwa vikitumika kuharibu ubora wa ngozi.**

**Kitaifa**

TANZANIA DAIMA.

# TADB yamwaga mikopo Zilagula

**NA MWANDISHI WETU, SENGEREMA**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) yatoa mkopo wa milioni 100.7 kwa Chama cha Ushirika cha Zilagula kilichopo Halmashauri ya Buchosa Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza.

Mkopo huo ni kwa ajili ya kununua zana bora za uvuvi zitakazowasaidia kuongeza mitaji, kupunguza upotevu wa samaki na kuongeza uthamani wake ili kuwanufaisha wavuvi na kukuza uchumi nchi.

Akizumgumza wakati akikabidhi hundi hiyo Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega alisema Serikali inataka kuona uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya wafugaji na wavuvi kupitia mikopo inayotolewa na Benki hiyo ili kuyaongezea thamani mazao yanayotokana na sekta za mifugo na uvuvi sambamba na kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi.

Aidha amewataka viongozi wa vyama vya ushirika kujiepusha na ubadhilifu wa fedha za mikopo hiyo kutoka TADB, huku akitoa rai kwa wavuvi kuwa na uchumi endelevu na hatimaye kuwa walinzi wa rasilimali za uvuvi kupitia vyama vyao vya ushirika.

Alisema azma ya serikali ni kuona Tanzania inaongoza kwa kusafirisha minofu ya samaki kwenda nje ya nchi na mchango wa samaki katika pato la taifa unaongezeka kutoka asilimia 1.7 hadi 2 ya sasa na kufikia asilimia tano na kuendelea.

Pia aliwataka watendaji wa serikali kutoa elimu kwa vyama vya ushirika namna ya kuitumia vyema mikopo wanayopata ili waweze kuirejesha kwa wakati pamoja na kuwaongoza ili waweze kupata mikopo mikubwa zaidi kwa kuwa utoaji mikopo kwa vyama vya ushirika vya wafugaji na wavuvi ni maono ya Rais John Magufuli.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaenda kuwa msimamizi namba moja wa vyama vya ushirika tena kwa barua, hivyo niwatakeni uongozi wa mkoa, halmashauri na ushirika wekeni taarifa zenu vizuri, tunataka viwanda vidogo vidogo vya wafugaji na wavuvi vikiwemo vya kukausha dagaa, minofu ya samaki na kutengeneza kayabo nzuri ili mpeleke bidhaa hizo kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi." alisema Ulega

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Mandeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) Japhet Justine aliwashukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuweka mikakati mizuri na benki hiyo ili kuhakikisha wafugaji na wavuvi wanakuwa na sifa za kupatiwa mikopo kwa ajili ya kuendeleza sekta hiyo.

"Tuliomba kwanza vyama hivi vikae katika ushirika kwa sababu tuliamini ule umoja wao utatupatia njia kuhakikisha mikopo inalipwa kwa kuwaweka katika mfumo ulio rahisi, wizara pia iliweka mazingira wezeshi ili benki iweze kuwa na taarifa sahihi ya mitumbwi ya wahusika wanaopatiwa mikopo,"anasema Justine.

Alivitaka vyama vya ushirika vilivyonufaika na mkopo waTADB kuhakikisha vinalipa mikopo hiyo kwa wakati ili watanzania wengine wenye uhitaji. waweze kupata na kukuza biashara zao.

Mratibu wa dawati la Sekta binafsi lililo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Steven Michael alisema kazi yao kubwa ni kuhakikisha matokeo chanya yanaonekana."Tumefanya kazi kubwa kuhakikisha vyama vya ushirika vinaunganishwa na taasisi za kifedha kupitia halmashauri mbalimbali nchini na kufuatilia mara kwa mara kuwa tunawaunganisha wadau wa sekta ya mifugo na uvuvi na taasisi hizo kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi," alisema Michael.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Crispin Luanda alisema kwa kutambua mchango wa sekta hiyo wametoa sh million 15 kutoka katika mapato yao ya ndani kwa vyama vitatu vya ushirika ambavyo ni Zilagula, Kasalazi na Soswa.




*Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega na Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine (wa pili kushoto), wakikikabidhi Chama cha Ushirika cha Zilagula wilayani Sengerema hundi ya mkopo wa Sh milionI 100.7 iliyotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kununua zana bora za uvuvi zitakazowasaidia kuongeza mitaji,kupunguza upotevu wa samaki mwishoni mwa wiki.*

## 'Tuwekeze katika viwanda vya ndani'

NIPASHE UK 9

# 'Ni aibu ofisi za serikali kutumia maziwa ya kopo'

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameziasa ofisi za serikali na wadau mbalimbali nchini, kutumia maziwa yanayozalishwa kupitia mifugo ya nchini badala ya kutumia ya kopo kutoka nchi za nje.

Ulega, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa, wakati akifungua maadhimisho ya Wiki ya Maziwa yaliyofanyika kitaifa mkoani Dodoma huku kilele cha maadhimisho hayo kikitarajiwa kufanyika Juni mosi, mwaka huu.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, unywaji wa maziwa yanayozalishwa nchini kutasaidia kuchochea na kuongeza uchumi wa taifa na kwa mwananchi mmoja mmoja.

"Ni aibu kubwa kwa ofisi za serikali kutumia maziwa ya kopo, nasema hivi kwa sababu hivi leo ukiingia katika ofisi za serikali utakuta maziwa ya kopo ndio yanatumika, kwa nini tusitumie maziwa yetu," alihoji Ulega.

Aliwataka wananchi kupenda na kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuzipatia soko yakiwamo maziwa ili kukuza uchumi wa nchi.

Pia, Ulega alisema takwimu zinaonyesha kuwa taifa liko chini katika suala la unywaji wa maziwa duniani kwa mwaka mtu mmoja anakunywa lita 54, wakati anatakiwa kunywa angalau lita 200.

Alifafanua kuwa kikanda takwimu zinaonyesha mtu mmoja anatakiwa kunywa lita 74 kwa mwaka wakati Tanzania upo uwezekano wa kuzalisha lita bilioni tatu kwa mwaka.

"Tanzania tuna uwezo wa kuzalisha lita bilioni tatu, kwa mwaka, lakini licha ya kuzalisha maziwa mengi na kuongoza kwa kuwa na mifugo mingi, lakini bado Watanzania wameonekana kuwa wavivu wa kunywa maziwa na wengine kuonekana kupendelea kunywa maziwa ya unga yanayozalishwa nchi za nje, hii ni aibu sana tuwe wazalendo Watanzania,"alisisitiza Ulega

Alisema, kama unywaji wa maziwa utazingatiwa ipasavyo kwa Watanzania wote uchumi wa viwanda na taifa kwa ujumla utaongezeka.

Alisema sekta ya maziwa, ni wezeshi kwa uchumi wa Taifa la Tanzania na hivyo jitihada zinatakiwa kufanyika kuhakikisha unywaji wa maziwa unazingatiwa kwa Watanzania wote.

Kwa upande wake Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa, Dk. Sophia Mlote alisema, bodi hiyo imefanya mapitio ya sheria ya maziwa ya mwaka 2004, ili kuendana na kasi ya mahitaji ya sasa kwa lengo la kuwezesha Bodi ya maziwa kuchochea maendeleo katika mnyororo wa thamani.

Hata hivyo, alisema bodi hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya ukusanyaji na usafirishaji bidhaa hiyo.

Scanned with CamScanner